

Mtu akija kwangu naye HAMCHUKII baba yake hawezi kuwa
mwanafunzi wangu?

SWALI: Bwana Yesu alikuwa anamaanisha nini katika hivi vifungu?

Luka14:26 “kama mtu akija kwangu naye HAMCHUKII baba yake, na mama yake, na mke wake, na wanawe, na ndugu zake waume na wake; na naam, na hata nafsi yake mwenyewe , hawezi kuwa mwanafunzi wangu ”.

JIBU: Bwana Yesu aliposema yeye “*asiyemchukia*” baba yake na mama yake, hakumaanisha, kumdharaau, au kuweka uadui naye, hapana kwasababu Bwana Yesu hawezi kufundisha upande mmoja upendo na mwingine chuki, bali pale alimanisha kupenda mapenzi ya wazazi au ya mtu binafsi Zaidi ya mapenzi ya Mungu, mtu wa namna hiyo hawezi kuwa mwanafunzi wake.

Leo hii mtu atafahamu kabisa kuwa mlevi au kufanya matambiko ya kimila ni dhambi sawa sawa na Neno lake katika

Mtu akija kwangu naye HAMCHUKII baba yake hawezi kuwa
mwanafunzi wangu?

*Kumbukumbu 18:10 “Asionekane kwako mtu ampitishaye mwanawe
au binti yake kati ya moto, wala asionekane mtu atazamaye bao,
wala mtu atazamaye nyakati mbaya, wala mwenye kubashiri, wala
msihiri,*

*11 wala mtu alogaye kwa kupiga mafundo, wala mtu apandishaye
pepo, wala mchawi, wala mtu awaombaye wafu.*

*12 Kwa maana mtu atendaye hayo ni chukizo kwa Bwana; kisha ni
kwa sababu ya hayo Bwana, Mungu wako, anawafukuza mbele
yako.*

13 Uwe mkamilifu kwa Bwana, Mungu wako.

lakini kwasababu mzazi wake anamshurutisha afanye vile kwasababu wazee wa ukoo wameagiza ,na asipofanywa hivyo atatengwa na ukoo, ye ye anaamua awe mlevi, au apige ramli ili tu kuwaridhisha wazazi wake. Mtu wa namna hiyo biblia inasema hawezi kuwa mwanafunzi wa YESU.

Kadhalika Bwana anasema mtu asipozaliwa kwa maji na kwa Roho hawezi kuuona ufalme wa mbinguni, lakini mtu kwasababu dini ya wazazi wake haiamini hivyo, anaona vema abaki hivyo hivyo tu, angali akijua kabisa ubatizo sahihi ule wa kuzamishwa katika maji tele tena katika Jina la YESU KRISTO ndio Bwana anaouhitaji kwa mtu kwa ajili

Mtu akija kwangu naye HAMCHUKII baba yake hawezi kuwa
mwanafunzi wangu?

ya ondoleo la dhambi zake, lakini yeye hataki kutii akiwaogopa wazazi
au ndugu zake..Sasa mtu kama huyu hawezi kuwa mwanafunzi wa
YESU.

Na maagizo mengine yote Bwana aliyotupa, hatupaswi tutazame kwanza
wanadamu wanatoa maoni gani kuhusu hayo.Kama ni Bwana kasema
moja kwa moja tunatii pasipo kuwatazama wanadamu wanasema nini.

Ili kufanyika wanafunzi kweli kweli wa Kristo hatuna budi kuingia
gharama, Hivyo Bwana atupe rehema tuweze kuzishinda hatua zote.

Amen.

Ikiwa utahitaji msaada zaidi ya mafundisho ya kila
siku/maombezi/ubatizo/ushauri basi wasiliana nasi kwa namba zetu hizi
+255693036618/+2557890001312

Au jiunge na makundi yetu ya mafundisho ya kila siku kwa njia ya
Whatsapp kwa kubofya hapa >>> WHATSAPP GROUP

Mada zinazoendana:

Mtu akija kwangu naye HAMCHUKII baba yake hawezi kuwa
mwanafunzi wangu?

JE! NI KWELI UMEMFUATA YESU?

JIKANE NAFSI MTEULE WA MUNGU.

**UKIAMINI NA UKIMKIRI YESU KWA KINYWA CHAKO,
UTAOKOKA.**

UBATILI.

WANA WA MAJOKA.

RACA

Rudi Nyumbani:

Share on:
WhatsApp